

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOKETI TAREHE
24/11/2021 KWA AJILI YA KUJADILI NJIA ITAKAYOTUMIKA KATIKA
UJENZI WA MIRADI YA MAENDELEO YA UVICO-19, MIRADI YA
MWIBUYE, ICU NA MADARASA 52/57

WALIOHUDHURIA:

1. NURFUS AZIZ
2. JOHN M. WISTON
3. JULIUS BUBERWA
4. DR. PETER L. JANGA

SAHIHI



CHEO

- M/KITI
KATIBU
MJUMBE
MJUMBE

AGENDA:

1. Kufungua Kikao
2. Kujadili njia itakayotumika katika ujenzi wa miradi iliyotajwa
3. Mengineyo.
4. Kufunga Kikao

1. KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua Kikao kwa kuwaomba wajumbe wawe huru katika kuchangia mawazo yao juu ya agenda iliyopo mbele yao na kikao kilifunguliwa mnamo saa 7:30 mchana.

**2. KUJADILI NJIA ITAKAYOTUMIKA KATIKA UJENZI WA MIRADI
YA MAENDELEO YA UVICO-19, MRADI YA MWIBUYE, ICU NA
MADARASA 52/57.**

Katibu aliwasilisha ombi la kujadili njia itakayotumika katika ujenzi wa miradi ya Maendeleo ya UVICO 19, Mradi wa Mwibuye (Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi 3 in 1), ICU na ujenzi wa Madarasa 57. Katibu aliwasilisha njia ya FORCE ACCOUNT na wajumbe walipokea ombi hilo na kulijadili.

Pamoja na majadiliano, Katibu pia aliwasilisha mapokekezi ya fedha za miradi hiyo. Ambapo. ICU SH: 250,000,000.00, Mwibuye nyumba ya Mtumishi Sh:90,000,000.00, Madarasa 52 Sh: 1,140,000,000.00.


Wajumbe baada ya kujadiliana, walipitisha kwa pamoja njia hiyo iliyopendekezwa ya FORCE ACCOUNT pamoja na kupokea taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi hiyo.

KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa jinsi walivyokuwa chachu katika kuchangia mawazo yao yaliyopelekea kufanikisha agenda ya kikao hiki hatimaye alifunga kikao mnamo saa 10:47 jioni.



Nurfus Aziz,
Mwenyekiti wa Bodi.



John M. Wiston,
Katibu wa Bodi.